

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**



**TAARIFA KWA UMMA**

**AWAMU YA KWANZA YA WATUMISHI WA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI WAHAMIA DODOMA MAKAO MAKUU YA NCHI TAREHE 27 FEBRUARI, 2017**

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inapenda kuwafahamisha Umma kuwa, Awamu ya Kwanza ya Watumishi wa Wizara wamehamia Makao Makuu ya Nchi, Dodoma tarehe 27 Februari 2017.

Awamu ya kwanza inajumuisha Watendaji Wakuu wa Wizara akiwemo Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu.

Wamo pia baadhi ya Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na wasaidizi wao.

Aidha, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi pia inawajulisha kuwa kwa sasa Ofisi zetu zitakuwa katika majengo ya Asha Rose Migiro Foundation katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Anuani mpya itakayotumiwa mkoani Dodoma ni:

**Katibu Mkuu,  
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi,  
S.L.P 2916,  
DODOMA**

**Simu: +255 262323189/262320186**

Barua pepe: [ps@moha.go.tz](mailto:ps@moha.go.tz)

Website: [www.moha.go.tz](http://www.moha.go.tz)

Imetolewa na:

Christina R. Mwangosi

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali  
Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

28/2/2017